



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA



**TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA
WATAHINIWA WA MTIHANI WA UALIMU DARAJA
LA A (GATCE) 2021**

SAYANSI



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU SAYANSI NA TEKNOLOJIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA



**TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA
WATAHINIWA WA MTIHANI WA UALIMU DARAJA
LA A (GATCE) 2021**

632 SAYANSI

Imechapwa na:
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P 2624,
Dar es Salaam, Tanzania.

© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2021

Haki zote zimehifadhiwa.

YALIYOMO

DIBAJI.....	iv
1.0 UTANGULIZI.....	1
2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KWA KILA SWALI .	2
2.1 Sehemu A: Maswali ya Majibu Mafupi.....	2
2.1.1 Swali la 1: Upimaji	2
2.1.2 Swali la 2: Huduma ya Kwanza.....	4
2.1.3 Swali la 3: Mashine Rahisi	7
2.1.4 Swali la 4: Maandalizi ya Ufundishaji.....	10
2.1.5 Swali la 5: Mifumo ya Mwili.....	12
2.1.6 Swali la 6: Misingi ya Kufundishia Somo la Sayansi.....	14
2.1.7 Swali la 7: Maada	16
2.1.8 Swali la 8: Viumbe Hai.....	19
2.1.9 Swali la 9: Nishati.....	21
2.1.10 Swali la 10: Maada	24
2.2 Sehemu B: Insha	27
2.2.1 Swali la 11: Afya na Njia za Kujikinga na Magonjwa	27
2.2.2 Swali la 12: Nishati.....	32
2.2.3 Swali la 13: Mifumo ya Mwili.....	38
2.3 Sehemu C: Insha	43
2.3.1 Swali la 14: Usimamizi wa Maabara	43
2.3.2 Swali la 15: Upimaji	48
2.3.3 Swali la 16: Maandalizi ya Ufundishaji.....	52
3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU WA WATAHINIWA KATIKA KILA MADA	57
4.0 HITIMISHO	57
5.0 MAPENDEKEKEZO	58
Kiambatanisho cha pekee	60

DIBAJI

Baraza la Mitihani la Tanzania linapenda kutoa taarifa ya Uchambuzi wa Majibu ya Watahiniwa wa Mtihani wa Ualimu Daraja la A (Grade A Teacher Certificate Examinations – GATCE) kwa mwaka 2021 katika somo la Sayansi. Lengo la taarifa hii ni kutoa mrejesho kwa wakufunzi, wanachuo, wakuu wa vyuo, maafisa elimu, wadhibiti ubora na wadau wengine wa elimu juu ya namna watahiniwa walivyojibu maswali ya mtihani. Mrejesho huo utawawezesha kufahamu mafanikio pamoja na changamoto zinazowakumba watahiniwa katika ujifunzaji kupitia namna wanavyojibu mtihani na hivyo kutafuta mbinu za kutatua changamoto hizo.

Mtihani huu ni tathmini ya mwisho ambayo pamoja na mambo mengine inaonesha mafanikio katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Sayansi. Kimsingi majibu ya watahiniwa ni uthibitisho wa maarifa na ujuzi waliopata watahiniwa katika kipindi cha miaka miwili cha mafunzo ya Ualimu kwa ngazi husika. Kwa ujumla, ufaulu katika somo la Sayansi ulikuwa wa kiwango kizuri. Watahiniwa walionesha kuwa na uwezo mzuri katika kusoma na kuelewa matakwa ya swali. Aidha, walikuwa na maarifa ya kutosha katika mada zilizokuwa na ufaulu mzuri. Kwa upande mwengine, katika maswali yaliyokuwa na ufaulu hafifu, watahiniwa walionesha kukosa maarifa ya kutosha, kushindwa kubaini matakwa ya swali na wengine kushindwa kuandika katika mtiririko wenye mantiki kwa kutumia lugha fasaha.

Ni matumaini ya Baraza la Mitihani la Tanzania kuwa mrejesho wa taarifa hii utatoa picha halisi kwa wadau wa elimu kuhusu mwenendo wa ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Sayansi, hivyo kuchukua hatua stahiki zitakazolenga kuboresha kiwango cha ufaulu katika somo hilo kwa mitihani ijayo.

Mwisho, Baraza la Mitihani la Tanzania linatoa shukrani za pekee kwa maafisa mitihani, wakufunzi na wadau wote waliohusika katika kundaa taarifa hii.



Dkt. Charles E. Msonde

KATIBU MTENDAJI

1.0 UTANGULIZI

Karatasi ya mtihani wa somo la Sayansi ilikuwa na jumla ya maswali 16 yaliyogawanyika katika sehemu A, B na C. Sehemu A ilikuwa na maswali 10 ya majibu mafupi kutoka katika mada zenye maudhui ya taaluma na ufundishaji. Mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali yote. Kila swali lilikuwa na alama nne (4), hivyo kufanya jumla ya alama 40. Sehemu B na C zilikuwa na maswali matatu (3) ya insha kwa kila moja. Mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali mawili kutoka katika kila sehemu. Kila swali lilikuwa na alama 15, hivyo kufanya jumla ya alama 60 kutoka sehemu zote mbili. Maswali katika sehemu B yaliandaliwa kutoka katika mada za taaluma na sehemu C mada za ufundishaji.

Jumla ya watahiniwa 3,101 walifanya mtihani wa somo la Sayansi ambapo asilimia 99.84 walifaalu na asilimia 0.16 hawakufaulu. Kiwango hiki cha ufaulu kimepanda kwa asilimia 0.36 ikilinganishwa na mwaka 2020 ambapo asilimia 99.48 ya watahiniwa walifaalu.

Katika kuchambua takwimu za ufaulu kwa kila swali, viwango vitatu vya ufaulu vilitumika kwa kuzingatia asilimia ya watahiniwa waliofaulu katika swali husika. Kiwango hafifu kilianzia asilimia 0 hadi 39, kiwango cha wastani asilimia 40 hadi 69 na kiwango kizuri kuanzia asilimia 70 hadi 100. Watahiniwa waliopata kuanzia kiwango cha wastani hadi kizuri walihesabika wamefaulu swali husika. Aidha, rangi za kijani, njano na nyekundu zimetumika katika chati kuwakilisha kiwango kizuri, cha wastani na hafifu, mtawalia.

2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KWA KILA SWALI


Katika sehemu hii uchambuzi wa takwimu za ufaulu wa kila swali pamoja na majibu ya watahiniwa umefanyika. Mifano mbalimbali ya majibu ya watahiniwa waliojibu maswali vizuri au walioshindwa kujibu vizuri imetolewa. Aidha, katika kuelezea majibu hayo vielelezo ambavyo ni majibu kutoka kwenye skripti za watahiniwa vimetumika.

2.1 Sehemu A: Maswali ya Majibu Mafupi

Jumla ya maswali 10 yamechambuliwa katika sehemu hii. Kila swali lilikuwa na alama nne. Mfiko wa alama wa viwango vya ufaulu katika sehemu hii ni 0 – 1.5 kwa ufaulu hafifu, 2 -2.5 kwa ufaulu wa wastani na 3 – 4 kwa ufaulu mzuri. Uchambuzi wa maswali hayo ni kama ifuatavyo:

2.1.1 Swali la 1: Upimaji

Swali lilimtaka mtahiniwa kutoa hoja nne zinazoelezea umuhimu wa kutoa mazoezi ya darasani wakati wa mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Kwa ujumla swali hili lilikuwa na kiwango kizuri cha ufaulu kwani watahiniwa 3,087 (99.5%) walifaulu na watahiniwa 14 (0.5%) pekee ndio hawakufaulu. Muhtasari wa ufaulu wa watahiniwa katika swali hili umeoneshwa katika Chati Na. 1.



Chati Na. 1: Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 1.

Chati Na. 1 inaonesha kuwa, asilimia 98.9 ya watahiniwa walipata alama kuanzia 3 hadi 4, asilimia 0.6 walipata alama kuanzia 2 hadi 2.5 na asilimia 0.5 walipata alama kuanzia 0 hadi 1.5.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, watahiniwa wengi (99.5%) walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu umuhimu wa kutoa mazoezi ya darasani wakati wa mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji hivyo, walitoa hoja mbili hadi nne kwa usahihi. Kati yao, asilimia 95.9 walitoa hoja zote nne kwa usahihi na kufanya swali hili kuwa na ufaulu wa juu zaidi ikilinganishwa na maswali mengine. Watahiniwa walitoa hoja mbalimbali sahihi kama vile: *kuamsha ari ya kujifunza zaidi kwa mwanafunzi, humsaidia mwalimu kuboresha njia na mbinu za ufundishaji na ujifunzaji, humsaidia mwalimu kubaini mada zenye utata kwenye ufundishaji na ujifunzaji na humsaidia mwalimu kupima malengo mahsus kama yamefikiwa.* Majibu hayo yanaonesha kuwa watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana ya upimaji hususan umuhimu wa kutoa mazoezi ya darasani wakati wa ufundishaji na ujifunzaji. Kielelezo Na. 1.1 ni sampuli ya jibu sahihi lililotolewa na mmoja wa watahiniwa.

- | | |
|----|---|
| 1) | Humsaidia mwalimu kyuwa changamoto za wanajunzi katika ufundishaji na ujifunzaji |
| 2) | Kumsaidia mwalimu kuboresha zana, na mbinu za kuendeshia na kujifunzia |
| 3) | Kumsaidia mwalimu kyuwa maendeleo ya kila mwanajunzi darasani |
| 4) | Humsaidia mwalimu kyuwa kufikiwa au kutefikiwa kwa malingo ya vomo kutoka na mtaala |

Kielelezo Na. 1.1: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 1.

Katika Kielelezo Na. 1.1 mtahiniwa alitoa hoja nne kwa usahihi zinazolezea umuhimu wa kutoa mazoezi darasani.

Hata hivyo, watahiniwa wachache (0.5%) walishindwa kujibu swali hili kwa usahihi. Baadhi yao, walitoa hoja ambazo hazihusiani na umuhimu wa kutoa mazoezi wakati wa ufundishaji na wengine walitoa hoja moja tu

sahihi. Baadhi ya majibu yasiyo sahihi yaliyotolewa ni kama vile: *kujua watoro na waliohudhuria, kuondoa hofu, kuwasaidia waelewe na kumsaidia mwalimu kufundisha kwa kujiamini*. Majibu haya si sahihi kwani mwalimu hutumia daftari la mahudhurio kujua waliohudhuria na wasiohudhuria. Pia, mwalimu hutumia mbinu mbalimbali shirikishi ili kuwasaidia wanafunzi waelewe na kuwaondolea hofu. Halikadhalika, mwalimu hufanya maandalizi ya ufundishaji kama vile kuandaa mbinu bora ya kufundishia, zana na vifaa vingine ambavyo humfanya afundishe kwa kujiamini na sio kwa kutegemea mazoezi ya darasani. Aidha, watahiniwa wengine waliandika majibu mafupi ambayo hayaendani na umuhimu wa kutoa mazoezi darasani. Majibu hayo ni kama vile: *kujitathmini, kuwapima, kuwasahihisha na kujiamini*. Kielelezo Na.1.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili kwa usahihi.


01.	<i>la Inamsaidiu mwanafunzi kahika ududisi</i>
05	<i>Inamsaidiu mwanafunzi kahika kuongezu mafupi</i>
10	<i>Inamsaidiu mwanafunzi kahika kupua mbinu za mawasiliano</i>
15	<i>Inamsaidiu mwanafunzi kahika kujiamini</i>

Kielelezo Na. 1.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 1.

Katika Kielelezo Na. 1.2, mtahiniwa aliandika matokeo ya matumizi ya mbinu bora za kufundishia/kujifunzia badala ya umuhimu wa kutoa mazoezi darasani.

2.1.2 Swali la 2: Huduma ya Kwanza

Swali lilimtaka mtahiniwa kueleza kwa ufupi mambo manne ya kuzingatia wakati wa kutoa huduma ya kwanza kwa mhanga wa ajali au kuugua. Swali lilikuwa na kiwango cha wastani cha ufaulu kwani watahiniwa 1,966 (63.4%) walifafulu na watahiniwa 1,135 (36.6%) hawakufaulu. Mchanganuo wa ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ni kama unavyoonekana katika Chati Na. 2.



Chati Na. 2: Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 2.

Chati Na. 2 inaonesha kuwa, asilimia 11.2 ya watahiniwa walipata alama kuanzia 3 hadi 4, asilimia 52.2 walipata alama 2 hadi 2.5 na asilimia 36.6 walipata alama kuanzia 0 hadi 1.5.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, watahiniwa (63.4%) waliojibu vizuri swali hili waliweza kueleza kwa ufupi mambo mawili hadi manne ya kuzingatia wakati wa kutoa huduma ya kwanza kwa mhanga wa ajali au kuugua. Baadhi ya majibu sahihi yaliyotolewa na watahiniwa ni kama vile: *Kumchunguza mhanga ili kupata uhakika wa tatizo utakalolishughulikia, Kuchunguza mazingira ya ajali ikiwa ni salama kuendelea kutolea huduma, Kuvalaa mipira mikononi (gloves) iwapo mhanga anatoka damu au majimaji yoyote, Kufahamu hatua zote muhimu za kumhudumia mhanga wa tatizo ulilibaini ili kuepuka kukuza tatizo au kumuongezea maumivu, Kuhakikisha umeandaa vifaa vyote vinavyotakiwa katika kutoa huduma ya kwanza iliyokusudiwa, Kumfariji mhanga ili kumuondolea wasiwasi kuhusu ukubwa wa tatizo lake.* Majibu hayo na yaliyooneshwa katika Kielelezo Na. 2.1 yanathibitisha kuwa, watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana ya huduma ya kwanza.

2. (i) kuzingatia sehemu sahihi kua jili ya kutoa
huduma ya kwanza
- (ii) Vifaa vya kutoea huduma ya kwa
naa mfano Bandago, Mkasi, glo
vsi na Pamba. Hili pia hi
jambo la kuzingatia ambapo Unapa
sue kuzingatia vifaa iti kuvuenda
kufimini huduma hivyo.
- (iii) Kumpa mgongwa Matumaini na -
kumpa dauer Jea kuthubza Naumi
vu. Hili ni moja wapo la jambo
la kuzingatia ambapo tunata kqua-
tuo madeno yenye kumpa mukhudumia
matumaini ili afisi kio faraja.
- (iv) Hili ya mgongwe kama harina-
endelea vibaya mpeleke kuq da
ktali, hili pia ni jambo la kuzi-
ngatia ili kuenda kipotu mafabu zaidi

Kielelezo Na. 2.1: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 2.

Katika Kielelezo Na. 2.1 mtahiniwa alieleza kwa usahihi mambo manne ya kuzingatia wakati wa kutoa huduma ya kwanza kwa mhanga wa ajali au kuugua.

Uchambuzi zaidi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, watahiniwa walioshindwa kujibu swali hili kwa usahihi walikosa umakini katika kusoma na kuelewa matakwa ya swali. Kwa mfano, wapo watahiniwa ambao waliandika hatua za kufuata unapomhudumia mhanga wa ajali, wengine walilisoma neno ‘kuugua’ kama ‘kuungua’ hivyo, waliandika hatua za kufuata katika kumhudumia mtu anayeungua moto. Mfano wa majibu hayo ni kama: *kumtoa katika moto au chanzo cha moto, kumlaza chini kwa haraka zaidi, kumfunika blanketi maalumu la kuzimia moto, mpake mhanga wa moto mafuta ya mgando au asali katika majeraha ya kuungua*. Pia, kuna watahiniwa ambao walieleza hatua za kutoa huduma ya kwanza kwa mhanga anayevuja damu kama vile: *kuosha jeraha kwa maji safi na sabuni, kumfunga sehemu ambayo imeumia ili kuzuia damu isivuje, kumpeleka hospitali*. Kielelezo Na. 2.2 ni sampuli ya jibu lisilo sahihi la mmoja wa watahiniwa.


d	<p>i) Kumketisha chini; hapa unatakuwa kumtuijiria chini mg'onyi huyu aliyejata afali. Mfano aliyeunjika mfupa</p> <p>ii) Kumbaa vitu vinaufo mbana katika mivilivake. Mfano bangili na nguo zetuombana.</p> <p>iii) Kumuweka vifunde vivili rya mbao kushto na kulei ili asyisikie maumivii.</p> <p>iv) Kumpeleka hospitali; baada ya kumpatia hadhira huyo unatakiwa kumpeleka mg'onyi wa hospitali ili akapate matebabu.</p>
---	---

Kielelezo Na. 2.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 2.

Katika Kielelezo Na. 2.2 mtahiniwa aliandika hatua za kufuata katika kumhudumia mtu aliyeunjika mfupa kinyume na matakwa ya swali la 2.

2.1.3 Swali la 3: Mashine Rahisi

Swali lililenga kupima uelewa wa watahiniwa kuhusu mashine za roda. Swali liliuliza: *Ni kwa namna gani roda tuli hutofautiana na roda huru?* Ufaulu katika swali hili ulikuwa wa kiwango kizuri kwani watahiniwa 2,786 (89.8%) walifaalu na watahiniwa 315 (10.2%) hawakufaulu. Ufaulu huo umeoneshwa kwa muhtasari katika Chati Na. 3.




Chati Na. 3: Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 3.

Chati Na. 3 inaonesha kuwa asilimia 77.8 ya watahiniwa walipata alama kuanzia 3 hadi 4 asilimia 12.0 walipata alama 2 hadi 2.5 na asilimia 10.2 walipata alama kuanzia 0 hadi 1.5.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa kati ya asilimia 89.8 ya watahiniwa waliofaulu kwa kupata alama mbili hadi nne, asilimia 71.5 waliweza kueleza kwa usahihi tofauti iliyopo kati ya roda tuli na roda huru hivyo kupata alama zote nne. Majibu sahihi yaliyotolewa na watahiniwa hao ni kama vile: *roda tuli ni aina ya roda ambayo gurudumu lake haliwezi kujongea mfano roda inayotumika kupandisha na kushusha bendera kwenye mlingotti. Wakati roda huru ni aina ya roda ambayo gurudumu lake hujongea mfano roda inayotumika kunyanyaua mzigoto bandarini.* Wengine waliandika: *roda huru hutumia jitihada kubwa kunyanyaua mzigoto mdogo wakati roda tuli hutumia jitihada ndogo kunyanyaua mzigoto mkubwa.* Majibu hayo kutoka kwa watahiniwa na kama yalivyoonesha katika Kielelezo Na. 3.1 yanathibitisha kuwa, watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana ya mashine rahisi hususan mashine za roda.

03.	Roda tuli; Ni aina ya roda ambayo magurudumu yake hayajongei hayajongei wakati wa Kupandisha au Kushusha mzigoto. Roda tuli, Maranyingi huwa na gurudumu moja tu ambalo hujaidia Kupandisha au Kushusha mzigoto. Tazama Kielelezo trifutacho.

Roda huru; Ni aina ya roda ambayo magurudumu ya kire hawexa kujongea watatu. wa kupandisha au kushusha m^zigo. Roda hii hawa na magurudumu mawili au zaidi ambayo hulumitika kupandisha au kushusha M^zigo. Tazama kielelezo kufuafachoo.



Kielelezo Na. 3.1: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 3.

Kielelezo Na. 3.1 kinaonesha jibu la mtahiniwa ambaye alieleza tofauti iliyopo kati ya roda tuli na roda huru. Mtahiniwa aliweka michoro kwa ufanuzi zaidi.

Kwa upande mwingine, watahiniwa waliokosa swali hili, hawakuwa na maarifa ya kutosha katika kutofautisha roda tuli na huru na wengine hawakuelewa matakwa ya swali. Wengi wao waliandika kuhusu matumizi yake, ubora wake, umuhimu wake na ufanyaji kazi wake. Aidha, wengine hawakufahamu kuwa mashine za roda ni sehemu ya mashine rahisi ambazo zimeundwa kwa mashine moja tu. Wao walikuwa wakitofautisha kwa kuzingatia idadi ya mashine zinazounda roda hizo. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika: *roda tuli huwa na mashine mbili au zaidi lakini roda huru huwa na mashine/mtaimbo mmoja tu*. Kielelezo Na. 3.2 ni mfano zaidi wa jibu lisilo sahihi la mmoja wa watahiniwa.


03 kufanana kwa roda tuli na roda huru kunato kana na kurambiq zote zinatumia magunu dumu katika kuzunguka kuwake au kufanya kazi.

Kielelezo Na. 3.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 3.

Katika Kielelezo Na. 3.2 mtahiniwa aliandika mfanano uliopo kati ya roda tuli na roda huru badala ya kueleza tofauti iliyopo kati ya roda hizo.

2.1.4 Swali la 4: Maandalizi ya Ufundishaji

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kufafanua kwa ufupi sehemu zifuatazo za andalio la somo: (a) Jedwali la taarifa za awali, (b) Malengo mahsus, (c) Tathmini ya mwalimu na (d) Maoni. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri kwani watahiniwa 3,076 (99.2%) walifaulu na watahiniwa 25 (0.8%) hawakufaulu. Mchanganuo wa ufaulu huo ni kama unavyoonekana katika Chati Na. 4.



Chati Na. 4: Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 4.

Chati Na. 4 inaonesha kuwa, asilimia 98.4 ya watahiniwa walipata alama kuanzia 3 hadi 4, asilimia 0.8 walipata alama 2 hadi 2.5 na asilimia 0.8 walipata alama kuanzia 0 hadi 1.5.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, watahiniwa (99.2%) waliojibu swali hili kwa usahihi walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu andalio la somo hivyo, waliweza kufafanua kwa ufupi sehemu mbili hadi nne za andalio la somo walizoulizwa. Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu sehemu za andalio la somo, maarifa ambayo yaliwawezesha kuandika majibu sahihi kama vile: (a) *Jedwali la taarifa za awali ni sehemu ambayo taarifa muhimu za mwanzo kama vile idadi ya wanafunzi waliohudhuria, somo, darasa, idadi ya vipindi, na tarehe hujazwa,* (b) *Malengo mahsus ni sentensi zinazoeleza matarajio ya ujifunzaji kwa wanafunzi, pia hutumia vitenzi vinavyopimika kama kutaja, kueleza na kuchora,* (c) *Tathmini ya mwalimu ni kipengele ambacho mwalimu anaeleza sababu za somo kufanikiwa au kutofanikiwa kwa kuzingatia lengo mahsus na idadi ya wanafunzi walioelewa au kutoelewa,* (d) *Maoni ni kipengele ambacho mwalimu hutoa mapendekizo au hatua za*

kuchukua kulingana na somo lilivyofikiwa. Kielelezo Na. 4.1 ni sampuli ya jibu sahihi lililotolewa na mmoja wa watahiniwa.

4	<p>a) Jedwali la taarifa za awali ni jedwali linalonesha mambo au vitu vya mwanzo katika andalio la somo. Mfano Idadi ya wanafunzi, Tiba la Mwalimu, Tiba la somo, tarehe na Muda.</p> <p>b) Malengo mahususi ni taarifa zinazo kucudia a kufikiwa ndani ya kipindi wimoja au viwili mfano Ndani ya kipindi cha dakisika aro baini (40) kila mwanafunzi auweza = i) Kueleza dhana ya nishati</p> <p>c) Tathmini ya mwalimu ni uchunguzi anaofanyiwa na mwalimu baada ya kumaliza kufundisha ili kupata taarifa zitakizo muwezeza kufanya maamuzi yaliyosahihii katika somo hiki. Mfano Wanafunzi 45 kati ya wanafunzi 50 wao auweza kueleza dhana ya nishati kwa usahihii.</p> <p>d) Maoni ni nifikakati au mapendekezo ya mwilimmo baada ya kumaliza kufundisha. Mfano Nitendelea na kipengele kinachopata lakini kwa wale ambao hawakuweza nitendelega kutoa mazoezi ya mara kwa mara dararani ili na wao waawezee kuelewa.</p>
---	---

Kielelezo Na. 4.1: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 4.

Kielelezo Na. 4.1 kinaonesha majibu sahihi ya mtahiniwa ambaye alifafanua kwa kutoa mifano sahihi katika kila kipengele cha andalio la somo alichouliizwa.

Kwa upande mwingine, watahiniwa wachache (0.8%) waliokosa swali hili, hawakuwa na uelewa wa kutosha katika dhana ya maandalizi ya ufundishaji hususan kipengele cha andalio la somo. Baadhi yao katika kipengele (a) walichanganya dhana ya jedwali la taarifa za awali na jedwali la hatua za ufundishaji na ujifunzaji. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika: *Jedwali la taarifa za awali ni jedwali ambalo linaonesha hatua mbalimbali za ufundishaji na ujifunzaji ambazo ni utangulizi, kujenga umahiri, kuimarisha umahiri na hitimisho.* Pia, katika kipengele (b) watahiniwa hao walishindwa kufafanua dhana ya malengo mahususi. Baadhi yao walifafanua kwa usahihii lakini waliweka mifano kwa kutumia vitenzi visivyopimika kama vile: *kufahamu, kutambua, kuelewa na kujua.* Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika: *Malengo mahususi ni mambo yote yanayotarajiwa kufikiwa ndani ya kipindi kimoja au viwili mfano; ndani ya*

kipindi cha dk 40 kila mwanafunzi aweze kutambua aina za nishati. Hali kadhalika, katika kipengele (c) na (d) baadhi ya watahiniwa walichanganya dhana ya tathmini ya mwalimu na maoni hivyo, walieleza maoni kama tathmini ya mwalimu na kinyume chake. Kielelezo Na. 4.2 ni sampuli ya jibu lisilo sahihi la mmoja wa watahiniwa.


04	la Jedwali la taarifa za awali Ni jedwali vinavyohusiana na azimio la somo
lb	Maonii mahususi Ni yule mombi ambayo yapo katika maddi
lc	Tathmin ya mwalimu Ni kwa kiasi qani wanafunzi wanawake kutoka kutoka
ld	Maoni Ni kuhusu kufanua kuu somo

Kielelezo Na. 4.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 4.

Katika Kielelezo Na. 4.2 mtahiniwa alishindwa kufafanua sehemu za andalio la somo alizoulizwa kwa sababu ya kukosa maarifa katika dhana hizo. Kwa mfano, aliandika jedwali la taarifa za awali vinavyohusiana na azimio la somo badala ya kufafanua taarifa hizo kama sehemu ya andalio la somo.

2.1.5 Swali la 5: Mifumo ya Mwili

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kubainisha sehemu nne za neva ya mota. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa hafifu kwani watahiniwa 1,083 (34.9%) pekee ndio walifaalu. Kwa upande mwengine, watahiniwa 2,018 (65.1%) hawakufaulu. Mchanganuo wa ufaulu huo ni kama unavyoonekana katika Chati Na. 5.



Chati Na. 5: Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 5.

Chati Na. 5 inaonesha kuwa asilimia 16.8 ya watahiniwa walipata alama kuanzia 3 hadi 4 asilimia 18.1 walipata alama 2 hadi 2.5 na asilimia 65.1 walipata alama kuanzia 0 hadi 1.5.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, watahiniwa wengi (65.1%) waliokosa swali hili hawakuwa na maarifa ya kutosha katika dhana ya Mfumo wa Fahamu wa binadamu. Watahiniwa hao walishindwa kubainisha sehemu zinazounda neva ya mota. Majibu ya baadhi yao yalijikita katika kubainisha mgawanyo wa neva hiyo kwa kuandika: sehemu za neva ya mota ni *sehemu ya mbele inayopeleka taarifa, sehemu ya kati, sehemu ya mwisho na mfereji*. Pia, watahiniwa wengine walibainisha aina za neva za fahamu kama vile: *neva ya mota, neva ya rilei na neva ya sensori*. Aidha, wapo ambaeo walitaja milango ya fahamu kama: *macho, ulimi, ngozi, pua na sikio*. Na wengine walitaja ogani zinazopatikana ndani ya mwili wa binadamu kama vile: *figo, ini, mapafu na moyo* badala ya kubainisha sehemu za neva ya mota. Kielelezo Na. 5.1 ni sampuli ya jibu lisilo sahihi la mmoja wa watahiniwa.

5.	i) neva ya palmoneli
	ii) neva ya gata
	iii) neva ya ateni
	iv) neva ya vena

Kielelezo Na. 5.1: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 5.

Katika Kielelezo Na. 5.1 mtahiniwa alichanganya dhana ya mfumo wa damu na mfumo wa fahamu. Hivyo aliandika mishipa ya damu badala ya kuandika sehemu za neva ya mota.

Hata hivyo, takriban theluthi moja ya watahiniwa (34.9%) waliojibu swalii hili kwa usahihi walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mfumo wa fahamu wa binadamu. Watahiniwa hao waliweza kubainisha sehemu mbili hadi nne za neva ya mota kwa usahihi. Sehemu hizo ni kama vile: *Kiini cha nyuroni*, *Seli*, *Dendraiti*, *Aksoni* na *Misuli*. Kielelezo Na. 5.2 kinaonesha sampuli ya jibu sahihi la mmoja wa watahiniwa.


5r	(i) <i>Aksom</i>
	(ii) <i>Dentiraiti</i>
	(iii) <i>nyukelia</i>
	(iv) <i>Saitoplazm</i>

Kielelezo Na. 5.2: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 5.

Kielelezo Na. 5.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa ambaye alibainisha kwa usahihi sehemu nne za neva ya mota.

2.1.6 Swali la 6: Misingi ya Kufundishia Somo la Sayansi

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kutoa hoja nne zinazoelezea umuhimu wa kujifunza somo la Sayansi. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri kwani watahiniwa 2,947 (95.0%) walifaalu na watahiniwa 154 (5.0%) hawakufaulu. Ufaulu huo umeonesha kwa muhtasari katika Chati Na. 6.



Chati Na. 6: Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 6.

Chati Na. 6 inaonesha kuwa, asilimia 80.3 ya watahiniwa walipata alama kuanzia 3 hadi 4, asilimia 14.7 walipata alama 2 hadi 2.5 na asilimia 5.0 walipata alama kuanzia 0 hadi 1.5.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, watahiniwa wengi (95.0%) walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu umuhimu wa somo la Sayansi hivyo, waliweza kutoa hoja mbili hadi nne za kueleza umuhimu wa kujifunza somo hilo. Kati yao, asilimia 55.7 waliweza kutoa hoja zote nne kwa usahihi. Baadhi ya majibu yaliyotolewa na watahiniwa hao ni kama vile: *husaidia kupata maarifa, stadi na ujuzi katika somo la Sayansi, husaidia kujenga mwelekeo chanya kuhusu somo la Sayansi, husaidia kuelewa na kutumia michakato ya kisayansi katika maisha ya kila siku, husaidia kutatua na kukabiliana na changamoto mbalimbali katika maisha, husaidia kupata wataalamu katika fani mbalimbali mfano wataalamu wa tiba, kilimo na uhandisi, husaidia kubuni na kutengeneza vifaa mbalimbali mfano kompyuta, simu na Tv.* Kielelezo Na. 6.1 kinaonesha sampuli ya jibu sahihi la mmoja wa watahiniwa katika swali hili.

6.	<p>i) Husaidia kujinga namna vunyeze kai wanayo tegengeana befilea Mazingira yao.</p> <p>ii) Husaidia namna ya kujinga na megingiwa Mbali nchali.</p> <p>iii) Husaidia kujinga namna wa kujinga na mazingira.</p> <p>iv) Husaidia kujinga namna ogani za mivili zinawashe fanya kazi nifano ogeni ya Moja.</p>
----	--

Kielelezo Na. 6.1: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 6.

Kielelezo Na. 6.1 kinaonesha jibu la mtahiniwa ambaye aliweza kueleza kwa usahihi umuhimu wa somo la Sayansi katika mazingira mbalimbali.

Kwa upande mwingine, watahiniwa wachache (5.0%) waliokosa swali hili walishindwa kuchanganua umuhimu wa somo la sayansi katika mzingira mbalimbali. Kati yao asilimia 4.1 walitoa hoja moja kwa usahihi na hivyo kupata alama moja. Baadhi yao waliandika jibu moja na kulirudia kwa namna tofauti wakidhani wanatoa majibu tofauti. Kwa mfano: *husaidia kupata wataalamu wa afya, husaidia kupata wahandisi, husaidia kupata bwana shamba, husaidia kupata wataalamu wa madawa.* Pia, wengine

waliandika majibu yasiyo sahihi kama vile: *mwanafunzi aweze kufaulu mtihani wa Sayansi* kuashiria kukosa maarifa ya kutosha kuhusu umuhimu wa somo hilo. Kielelezo Na. 6.2 ni sampuli ya jibu lisilo sahihi la mmoja wa watahiniwa.


6	<p>a) Humaidia mwanafunzi kujua uchunguzi wa kisayansi</p> <p>b) Humaidia mwanafunzi kujua maana ya maada</p> <p>c) Humaidia mwanafunzi kujua kusharabiwa kwa santi</p> <p>d) Humaidia mwanafunzi kufuhamu jinsi ya kupinda na kushara biwa kwa mwanga</p>
---	--

Kielelezo Na. 6.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 6.

Katika Kielelezo Na. 6.2 mtahiniwa aliandika dhana zinazopatikana/zinazofundishwa katika somo la Sayansi badala ya kueleza umuhimu wa kujifunza somo hilo.

2.1.7 Swali la 7: Maada

Swali la 7 lilimtaka mtahiniwa kubainisha hatua nne za kufuata unapounda fomula ya kampaundi ya kloraidi ya kalsiamu. Ufaulu wa jumla wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa wa kiwango hafifu kwani watahiniwa 660 (21.3%) pekee ndio waliofaulu. Kwa upande mwengine, watahiniwa 2,441 (78.7%) hawakufaulu. Mchanganuo wa ufaulu huo umeoneshwa kwa muhtasari katika Chati Na. 7.



Chati Na. 7: Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 7.

Chati Na. 7 inaonesha kuwa, asilimia 16.3 ya watahiniwa walipata alama kuanzia 3 hadi 4, asilimia 5.0 walipata alama 2 hadi 2.5 na asilimia 78.7 walipata alama kuanzia 0 hadi 1.5 .

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, asilimia kubwa (78.7%) ya watahiniwa walishindwa kubaini hatua za kufuata wakati wa kuunda fomula ya kampaundi. Kati yao, asilimia 70.0 walipata alama 0. Watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana ya simboli, valensi na fomula za elementi na kampaundi. Baadhi yao waliweza kuandika hatua stahiki lakini walishindwa kubaini elementi zinazounda kampaundi hiyo, simboli na valensi zake. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika: *hatua I, andika simboli za elementi ulizopewa ambazo ni Kalsiamu (K) na Klorini (Cl)*. Mtahiniwa huyu badala ya kuandika simboli ya kalsiamu ambayo ni Ca, aliandika simboli ya potasiamu ambayo ni K. Wengine walishindwa kuandika valensi za elementi husika kwa usahihi, hivyo kushindwa kuunda kampaundi ya CaCl_2 . Aidha, watahiniwa waliopata alama 0 walionesha kutofahamu kabisa namna ya kuunda kampaundi ya elementi. Wengi wao walijikita zaidi katika kuandika mambo mbalimbali yanayohusiana na dhana za elemeti, simboli, valensi na fomula ingawa hayana uhusiano wowote katika kujifunza dhana hizo. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika: *kuangalia namba ya atomi ya kila elementi, kuangalia valensi ya kila atomi, kuangalia idadi ya sheli ya kila atomi, kuangalia atomi za kila kundi katika jedwali mrudio la elementi*. Mwingine aliandika: *kutambua makundi ya elementi, kutambua valensi za elementi, kutambua majina ya elementi na kuandaa fomula za misombo*, na mwingine aliandika: *uwezo wa elementi kupambana kikemikali, uwezo wa elementi husika kuzalisha nishati, uwezo wa elementi kupoteza au kuongeza chaji na kutambua radikali ya elementi husika*. Kielelezo Na. 7.1 ni sampuli ya jibu lisilo sahihi la mmoja wa watahiniwa.

7.	i) Kuandaa vifaa 'zama vile kemikali'
	ii) Kuanza kutengeneza fomula
	iii) Kubalansce okwesheni
	iv) Kurhakikisha imekaa vizuri ilawesheni

Kielelezo Na. 7.1: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 7.

Katika Kielelezo Na. 7.1 mtahiniwa aliandika hatua za kuunda fomula katika maabara kwa kutumia kemikali na vifaa badala ya kuunda kwa kutumia simboli na valensi za elementi husika.

Kwa upande mwingine, watahiniwa (21.3%) waliojibu vizuri swali hili walikuwa na maarifa ya kutosha katika dhana ya simboli, valensi na fomula za elementi na kampaundi. Watahiniwa hao, walitumia maarifa hayo katika kubainisha hatua mbili hadi nne za kufuata unapokuwa unaunda fomula ya kampaundi ya kloraidi ya kalsiamu. Kati yao, asilimia 8.5 waliweza kuandika hatua zote nne ambazo ni: *Andika simboli za elementi zinazounda kampaundi hiyo yaani Ca na Cl, Andika valensi ya elementi upande wa juu wa kulia wa simboli hizo mfano Ca^2 na Cl^1 , Andika simboli hizo tena na zibadilishane valensi zao kwa kuziandika upande wa chini na kulia kwa simboli hizo mfano Ca_1 na Cl_2 , Baada ya kubadilishana valensi zake, ziunganishe kutoa fomula ya kampaundi ya Kloraidi ya Kalsiamu ambayo ni $CaCl_2$.* Kielelezo Na. 7.2 kinaonesha sampuli ya jibu sahihi lililotolewa na mmoja wa watahiniwa.


7. ① Andika simboli za elementi uliko Pewa yaani	Cl	Ca
② Andika valensi juu upande wa kulia leafika simboli za elementi hizo yaani:	Cl^1	Ca^2
③ Omesha namna zinavyo badilishwa valensi	Cl^-	Ca^2+
	Cl^-	Ca^2+
④ Andika formula bainili ya kompo undi nizi na yaa, kwa balanza na metali buingwidi si metali yaani: $CaCl_2$	$CaCl_2$	

Kielelezo Na. 7.2: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 7.

Katika Kielelezo Na. 7.2 mtahiniwa aliweza kubainisha simboli za elementi zinazounda kampaundi aliyopewa kuwa ni Ca na Cl, kisha aliandika valensi sahihi za elementi hizo upande wa juu kulia katika simboli za elementi hizo (Ca^2 na Cl^1), alionesha namna elementi zinavyobadilishana valensi na hatimaye kuandika fomula kamili ya kampaundi hiyo (CaCl_2).

2.1.8 Swali la 8: Viumbe Hai

Swali lililenga kupima uelewa wa watahiniwa kuhusu dhana ya kutegemeana kwa viumbe hai. Swali liliuliza: *Ni kwa namna gani binadamu anawategemea wanyama wengine? Toa hoja nne.* Kwa ujumla swali hili likuwa na kiwango kizuri cha ufaulu kwani watahiniwa 2,816 (90.8%) walifaalu na watahiniwa 285 (9.2%) hawakufaalu. Muhtasari wa ufaulu katika swali hili umeoneshwa katika Chati Na. 8.



Chati Na. 8: Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 8.

Chati Na. 8 inaonesha kuwa, asilimia 82.9 ya watahiniwa walipata alama kuanzia 3 hadi 4, asilimia 7.9 walipata alama 2 hadi 2.5 na asilimia 9.2 walipata alama kuanzia 0 hadi 1.5.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, watahiniwa wengi (90.8%) walijibu kwa usahihi kwani walikuwa na maarifa ya kutosha katika dhana ya viumbe hai. Watahiniwa hao, waliweza kuhusianisha maarifa hayo na maisha ya kila siku ya binadamu, hivyo waliweza kutoa hoja mbili hadi nne juu ya namna binadamu wanavyotegemea wanyama wengine. Kati yao, asilimia 63.7 walitoa hoja zote nne kwa usahihi na kupata alama 4. Baadhi ya majibu yao yalikuwa: *Binadamu anawategemea wanyama pori kujipatia kipato kupitia sekta ya utalii. Binadamu hula wanyama wengine kama vile ngombe na mbuzi. Binadamu hutumia wanyama wengine kama*

chombo cha usafiri kwa kubebia mizigo kutoka eneo moja kwenda jingine mfano puna. Binadamu hutengeneza mavazi kwa kutumia ngozi za wanyama na manyoya ya sufu. Binadamu hutumia vinyesi vya wanyama kutengeneza nishati mbalimbali. Kielelezo Na. 8.1 kinaonesha sampuli ya jibu sahihi la mmoja wa watahiniwa.

z.i.	<i>Binadamu anauntonge mea wanyama kwa a kuweza kupata kutewa chakula mfano unapokutuwa unamchijia ng'ombe, unapata ny ma na hio nyama ni chakula.</i>
ii.	<i>Binadamu anauntengemea unayimo kwa kuyiweka ulinzi m walama, pia kati ka m azingira yetu unakuto binadamu amfuga - wanyama kama vile mbwa, ng'o paka.</i>
iii.	<i>Binadamu anauntengemea unayamo kuxaji li ya kuyipatia mbolea mashambani, mfano kwa kuyipitia vile, vinyeti vya unayamo ko ma ng'ombe, kuku mbuzi ni mboleo marha mbani</i>
iv.	<i>Binadamu anauntengemea unayamo kux ajili ya kuyipatia ngozi, pia binadamu ana kuwa anahtegemea nyama kwa kupata ego zi ambayo hutumika kutengeneza vitu mbele mbali kama viadu.</i>

Kielelezo Na. 8.1: Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 8.

Kielelezo Na. 8.1 kinaonesha jibu la mtahiniwa ambaye alieleza namna binadamu anavyowategemea wanyama wengine katika chakula, ulinzi, mbolea na ngozi kwa ajili ya kutengeneza bidhaa mbalimbali.

Uchambuzi zaidi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, asilimia 9.2 ya watahiniwa hawakufanya vizuri katika swali hili, Baadhi yao, hawakufuata matakwa ya swali kwani walijikita katika kueleza mfanano uliopo kati ya binadamu na wanyama wengine kwa kuzingatia sifa za vimbe hai na tabia za wanyama na binadamu. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika: *binadamu hujongea na wanyama wengine pia hujongea, binadamu huzaliana na wanyama wengine huzaliana n.k.* Wengine waliandika majibu sahihi lakini walishindwa kujenga hoja ili kuleta maana

halisi. Mfano, mtahiniwa mmoja aliandika: *binadamu wanawategemea wanyama katika kustawisha mazao yao, katika kupata chakula, na katika shughuli za kilimo na uvuvi*. Mtahiniwa mwingine alitoa majibu yanaonesha kukosa maarifa katika dhana ya viumbe hai kwa kuandika: *binadamu wanategema wanyama kwa sababu wao wanatoa hewa ya kabondayoksaidi na kuvuta hewa ya oksijeni* wakati binadamu na wanyama wote wanavuta hewa ya oksijeni. Kielelezo Na. 8.2 ni sampuli jibu lisilo sahihi la mmoja wa watahiniwa.


8.	<ul style="list-style-type: none"> i. Binadamu hutumia hewa ya oksijeni na wanyama hutumia oksijeni. ii. Binadamu ana clamu na seli pia wanyama w ana selina clamu. iii. Binadamu hupata marachhi mbalimbali na wanyama nao hupata marachhi. iv. Binadamu huta wanyama na wanyama huta binadamu.
----	--

Kielelezo Na. 8.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 8.

Katika Kielelezo Na. 8.2 mtahiniwa aliandika mfanano uliopo kati ya binadamu na wanyama badala ya kueleza namna binadamu anavyowategemea wanyama wengine katika kuishi.

2.1.9 Swali la 9: Nishati

Swali la 9 lililenga kupima uelewa wa watahiniwa kuhusu vifaa vinavyounda sakiti ya umeme. Swali liliuliza: *Eleza kwa kifupi kazi za vifaa vifuatavyo kwenye sakiti ya umeme;* (a) *Amita*, (b) *Voltimita*, (c) *Waya na* (d) *Betri*. Kwa ujumla swali hili lilikuwa na kiwango kizuri cha ufaulu kwani watahiniwa 2,899 (93.5%) walifaalu na watahiniwa 202 (6.5%) hawakufalu. Muhtasari wa ufaulu wa watahiniwa katika swali hili umeoneshwa katika Chati Na. 9.



Chati Na. 9: Ufaulu wa watahiniwa katika swalii la 9.

Chati Na. 9 inaonesha kuwa, asilimia 45.7 ya watahiniwa walipata alama kuanzia 3 hadi 4, asilimia 47.8 walipata alama 2 hadi 2.5 na asilimia 6.5 walipata alama kuanzia 0 hadi 1.5.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, watahiniwa wengi (93.5%) walijibu swalii hili kwa usahihi kwani walikuwa na maarifa ya kutosha katika dhana ya nishati ya umeme, hivyo waliweza kueleza kwa usahihi kazi za vifaa viwili hadi vinne walivyopewa. Kati yao, asilimia 14.9 waliweza kueleza kazi ya vifaa vyote vinne kwa usahihi kama ifuatavyo: (a) *Amita ni kifaa kinachopima mkondo wa umeme katika kizio cha Ampia (A)*, (b) *Voltimita ni kifaa kinachopima volteji (tofauti ya potenshali) katika kizio cha volti (V)*, (c) *Waya ni kifaa kinachopitisha umeme kutoka kwenye chanzo kwenda kwenye vifaa vinavyotumia umeme na* (d) *Betri ni kifaa kinachotumika kama chanzo cha umeme katika sakiti ya umeme*. Kielelezo Na. 9.1 ni sampuli ya jibu sahihi la mmoja wa watahiniwa.

9.	<p>(a) Amita Ni kifaa katika sakiti ya umeme kifaa hiki hupima mkondo wa umeme katika kizidha Ampere.</p> <p>(b) Voltimita Ni kifaa katika sakiti ya umeme kifaa hiki hupi imsi Voltaji katika kizidha vodi (V).</p> <p>(c) Nitaku Ni kifaa katika sakiti ya umeme kifaa hiki hupi kishe Electroni kutoka katika chanzo cha umeme hadi kwonye tao.</p> <p>(d). Betri Ni kifaa katika sakiti ya umeme kifaa hiki upi hufaa chafu amri ngumu za umeme ili kuwazeha kifaa vingine kufonye kari na ndiyo chanzo cha umeme katika Sakiti.</p>
----	--

Kielelezo Na. 9.1: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 9.

Kielelezo Na. 9.1 kinaonesha majibu sahihi ya mtahiniwa ambaye alieleza kwa usahihi kazi za vifaa vyote vinne vya umeme alivyoulizwa.

Pamoja na ufaulu mzuri katika swali hili, watahiniwa wachache (6.5%) walishindwa kueleza kazi ya vifaa vyote vinne ama kuweza kueleza kazi ya kifaa kimoja tu, hivyo kupata alama moja au sifuri. Watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha katika dhana ya nishati ya umeme hususan sakiti ya umeme. Baadhi yao walichanganya matumizi ya vifaa hivyo katika sakiti ya umeme. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika: *Amita ni kifaa kinachopima tofauti ya potenshali. Voltimita ni kifaa kinachopima mkondo wa umeme. Waya ni kifaa kinachotunza umeme. Betri ni kifaa kinachoruhusu umeme kuwaka.* Aidha, watahiniwa wengine walichora alama za vifaa hivyo kwenye sakiti ya umeme badala ya kueleza kazi zake. Pia, wengine walichanganya dhana ya vifaa katika sakiti ya umeme na vizio vyake kwa kuandika: *Amita ni kizidha cha mkondo wa umeme. Voltimita ni kizidha cha tofauti ya potenshali kwenye sakiti.* Kielelezo Na. 9.2 ni sampuli ya jibu lisilo sahihi la mmoja wa watahiniwa.

a) Amita - Huhumika kuvalisha murung'a
b) Voltimita - huhumika kuenklesha murung'a kuperita -
c) Waya - kuinganisha amita ili tagi iweze kuwaka
d) Betri - Huhumika kuwasha taa

Kielelezo Na. 9.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 9.


Katika Kielelezo Na. 9.2 mtahiniwa alieleza kazi za vifaa hivyo katika kuzalisha nishati ya mwanga badala ya nishati ya umeme kama matakwa ya swali.

2.1.10 Swali la 10: Maada

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kusawazisha mapambano ya kikemikali yafuatayo:

- (a) $H_2SO_4 + CuO \rightarrow CuSO_4 + H_2O$
- (b) $NaOH + H_2SO_4 \rightarrow Na_2SO_4 + H_2O$
- (c) $Mg + HCl \rightarrow MgCl_2 + H_2$
- (d) $H_2SO_4 + NaHCO_3 \rightarrow Na_2SO_4 + H_2O + CO_2$

Swali hili lilikuwa na kiwango cha wastani cha ufaulu kwani watahiniwa 1,573 (50.7%) walifaulu na watahiniwa 1,528 (49.3%) hawakufaulu. Muhtasari wa ufaulu katika swali hili umeoneshwa katika Chati Na. 10.




Chati Na. 10: Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 10.

Chati Na. 10 inaonesha kuwa, asilimia 39.9 ya watahiniwa walipata alama kuanzia 3 hadi 4, asilimia 10.8 walipata alama 2 hadi 2.5 na asilimia 49.3 walipata alama kuanzia 0 hadi 1.5.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, watahiniwa (50.7%) waliojibu vizuri swali hili walikuwa na uelewa wa kutosha juu ya dhana ya maada hususan kipengele cha kusawazisha mapambano ya

kikemikali. Walifahamu kuwa, ili mpambano wa kikemikali uwe katika msawazo ni lazima idadi ya atomi za elementi husika ziwe sawa pande zote. Kati yao, asilimia 19.5 pekee ndio waliweza kusawazisha mapambano yote manne kwa usahihi na kupata alama nne. Kielelezo Na. 10.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyesawazisha mapambano yote manne kwa usahihi.



Kielelezo Na. 10.1: Sampuli ya jibu sahihi katika swalii la 10.

Katika Kielelezo Na. 10.1 mtahiniwa aliweza kubaini kuwa mpambano uliopo katika sehemu (a) ya swalii uko katika msawazo. Katika kipengele (b), aliweza kubaini kuwa upande wa kulia kuna atomi 2 za sodiamu hivyo, aliongeza atomi za sodiamu upande wa kushoto na baadae atomi za haidrojeni na oksijeni upande wa kulia ili kuweka mpambano katika msawazo. Halikadhalika, katika kipengele (c) alisawazisha kwa kuongeza idadi ya haidrojeni na klorini upande wa kushoto na (d) aliongeza idadi ya sodiamu, haidrojeni, kaboni na oksijeni upande wa kushoto na baadaye kulia.

Hata hivyo, asilimia 49.3 ya watahiniwa walishindwa kusawazisha mipambano yote ama kuweza kusawazisha mpambano mmoja tu hivyo kupata alama moja. Kati yao, asilimia 37.3 hawakuweza kusawazisha hata mpambano mmoja na kuishia kupata alama sifuri. Watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha katika dhana ya mapambano ya kikemikali hususan katika kusawazisha mapambano hayo. Baadhi yao walinakili milinganyo hiyo kama ilivyokuwa kwenye karatasi ya maswali. Aidha, watahiniwa wengine waliandika namba za molekyuli mbele ya kampaundi bila kuzingatia idadi ya atomi za upande wa kushoto na kulia. Jibu la mmoja wa watahiniwa lilikuwa kama ifuatavyo: (a) $\text{H}_2\text{SO}_4 + \text{CuO} \rightarrow \text{CuSO}_4 + 2\text{H}_2\text{O}$, (b) $\text{NaOH} + \text{H}_2\text{SO}_4 \rightarrow \text{Na}_2\text{SO}_4 + \text{H}_2\text{O}$, (c) $2\text{Mg} + \text{HCl} \rightarrow 2\text{MgCl}_2 + \text{H}_2$ na (d) $\text{H}_2\text{SO}_4 + 2\text{NaHCO}_3 \rightarrow \text{Na}_2\text{SO}_4 + \text{H}_2\text{O} + \text{CO}_2$.

Mtahiniwa huyo alikuwa akiongeza idadi ya atomu bila kuzingatia msawazo kwa pande zote mbili. Kwa mfano, katika kipengele (a), aliongeza atomi 2 za haidrojeni na oksijeni upande wa kulia hivyo kufanya haidrojeni 4 upande wa kulia na 2 upande wa kushoto. Kielelezo Na. 10. 2 ni mfano jibu lisilo sahihi kutoka kwa mmoja wa watahiniwa.

10. a. $\text{H}_2\text{SO}_4 + \text{CuO} \rightarrow \text{CuSO}_4 + \text{H}_2\text{O}$ formula $\text{H}_2\text{SO}_4 + \text{CuO} = \text{CuSO}_4 + \text{H}_2\text{O}$ $\text{H}_2\text{SO}_4 - \text{H}_2\text{O} = \text{CuSO}_4 - \text{CuO}$ $\text{SO}_4 = \text{CuSO}_4 - \text{CuO}$ $\text{SO}_4 = \frac{\text{CuSO}_4}{\text{SO}_4} - \text{CuO}$ CuO_2 $\therefore \text{H}_2\text{SO}_4 + \text{CuO} \rightarrow \text{CuSO}_4 + \text{H}_2\text{O} = \text{CuO}_2$.
b. $\text{NaOH} + \text{H}_2\text{SO}_4 \rightarrow \text{Na}_2\text{SO}_4 + \text{H}_2\text{O}$ formula $\text{NaOH} + \text{H}_2\text{SO}_4 = \text{Na}_2\text{SO}_4 + \text{H}_2\text{O}$ $\text{H}_2\text{SO}_4 - \text{H}_2\text{O} = \text{Na}_2\text{SO}_4 - \text{NaOH}$ $\text{H}_2\text{SO}_4 - \text{H}_2\text{O} = \text{Na}_2\text{SO}_4 - \text{NaOH}$ $\text{SO}_4 = \frac{\text{Na}_2\text{SO}_4}{\text{SO}_4} - \text{NaOH}$ $\text{Na}_2\text{O}\text{H}$ $\therefore \text{NaOH} + \text{H}_2\text{SO}_4 \rightarrow \text{Na}_2\text{SO}_4 + \text{H}_2\text{O} = \text{Na}_2\text{O}\text{H}$.
10.c. $\text{Mg} + \text{HCl} \rightarrow \text{MgCl}_2 + \text{H}_2$ formula $\text{Mg} + \text{HCl} = \text{MgCl}_2 + \text{H}_2$ $\text{Mg} - \text{MgCl}_2 = \text{H}_2 - \text{HCl}$ $\text{Cl}_2 = \text{H}_2 - \text{HCl}$ $\text{Cl}_2 = \text{H}_2$ $= \text{H}_2$ $\therefore \text{Mg} + \text{HCl} \rightarrow \text{MgCl}_2 + \text{H}_2 = \text{H}_2$.
d. $\text{H}_2\text{SO}_4 + \text{NaHCO}_3 \rightarrow \text{Na}_2\text{SO}_4 + \text{H}_2\text{O} + \text{CO}_2$ formula $\text{H}_2\text{SO}_4 + \text{NaHCO}_3 = \text{Na}_2\text{SO}_4 + \text{H}_2\text{O} + \text{CO}_2$ $\text{H}_2\text{SO}_4 - \text{H}_2\text{O} = \text{Na}_2\text{SO}_4 - \text{NaHCO}_3 + \text{CO}_2$ $\text{SO}_4 = \text{SO}_4 - \text{HCO}_3$ $\text{SO}_4 = \frac{\text{SO}_4}{\text{SO}_4} - \text{HCO}_3$ $\text{SO}_4 = \text{HCO}_3$ $= \text{HCO}_3$ $\therefore \text{H}_2\text{SO}_4 + \text{NaHCO}_3 \rightarrow \text{Na}_2\text{SO}_4 + \text{H}_2\text{O} + \text{CO}_2 = \text{HCO}_3$

Kielelezo Na. 10.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 10.


Katika Kielelezo Na. 10.2 mtahiniwa alisawazisha mapambano ya kikemikali aliyopewa kwa kutumia kanuni za hisabati kwani alirahisisha kwa kuondoa molekyuli zinazofanana badala ya kusawazisha idadi ya atomi upande wa kushoto na kulia.

2.2 Sehemu B: Insha

Jumla ya maswali matatu (3) yaliyoandaliwa kutoka katika mada za taaluma yamechambuliwa katika sehemu hii. Mfiko wa alama wa viwango vya ufaulu katika sehemu hii ni 0 – 5.5 ufaulu hafifu, 6.0 – 10.0 ufaulu wa wastani na 10.5 – 15 ufaulu mzuri. Uchambuzi wa maswali hayo ni kama ifuatavyo:

2.2.1 Swali la 11: Afya na Njia za Kujikinga na Magonjwa

Swali hili lililenga kupima uelewa wa watahiniwa kuhusu magonjwa ya kuambukiza na yasiyo ya kuambukiza. Swali liliuliza: *Si magonjwa yote husababishwa na viini vya magonjwa. Thibitisha kauli hii kwa kutumia hoja sita.* Jumla ya watahiniwa 2,790 (90.0%) walijibu swali hili kati yao, watahiniwa 2,003 (71.8%) walifaulu na watahiniwa 787 (28.2%) hawakufaulu hivyo kufanya swali hili kuwa na ufaulu mzuri. Mchanganuo wa ufaulu wa watahiniwa katika swali hili umeoneshwa kwa muhtasari katika Chati Na. 11.



Chati Na. 11: Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 11.

Chati Na. 11 inaonesha kuwa, asilimia 32.6 ya watahiniwa walipata alama kuanzia 10.5 hadi 15, asilimia 39.2 walipata alama 6 hadi 10.0 na asilimia 28.2 walipata alama kuanzia 0 hadi 5.5.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, watahiniwa (71.8%) waliopata alama za juu, walikuwa na maarifa ya kutosha katika mada ya Afya na Njia za Kujikinga na Magonjwa kwani waliweza kutoa hoja tatu hadi sita zinazothibitisha kuwa si magonjwa yote husababishwa na viini nya magonjwa. Watahiniwa hao waliweza kubaini kuwa magonjwa ya kuambukiza huenezwa na viini nya magonjwa wakati magonjwa yasiyoambukiza hayaenezwi na viini nya magonjwa bali hutokana na sababu mbalimbali kama vile: *kukosa lishe bora, urithi wa vinasaba nya magonjwa, mfumo mbaya wa maisha kama matumizi ya pombe, kemikali na madawa ya kulevyo, umri, magonjwa ya akili na magonjwa yatokanayo na mabadiliko ya mazingira*. Kielelezo Na. 11.1 ni sampuli ya jibu sahihi kutoka kwa mmoja wa watahiniwa.

11. Magonjwa, Ni Maadui ya langa
ya mirehi yanejo nifanya ritu adhefles
kafay, lembih na kulese nguru, Mago
ngwa huwa yeng heinbu kungu ya mirehi
na buifeny. Seti hei nyepenging prejona
na magonywa bukesangutu. Sio raweli
kwamba di Magonjwa yoke husatbabishu
na vii ni aya Magonywa, hii ni kwa Saber
bu viro usababishi mengine ya mago
ngwa mbali na viini ya magonywa, usq
babishi hinys ni;

LiShe deni; Mfano wa magonywa
ni, Rore, bilibatumby Metege, hayo mudjo
nywe huwe Sababishi na ritu kapo
te sone cha kuta cha cina fulmi kuq
mitgi na bukesq charule cha metandu
mengine kana, kliba tumbu huwa ni
Mfano amepata yatakuwengi
song nyenye asili ya twanga

Urithi Mfano wa Magonywa ni
kana vige, tsulatati, sitoseti Janemue,
magonywa hayo nibikiri bali magonywa
nyapeta buketene na urithi shwo bala
ta blua warazi weko wa baburabe
wa ukoo wabe:

Matumizi ya kerukali; Mfano
wa magonywa ni okosa ya ngoro, Mfano
kipilia Na funzi yahyo Urithi ya
lipodori hasa kuq isorawalek weke,
kipata magonywa kana hayo padpo
kuambuki rewa malali popote,

11

Ajari, Mfano metatizo ya Moyos
au figo Jipie Welencia, mchanga kwenye
kumpata ugonjwa wa namna aya pasipo
kingihwe mo imelaa ugonjwa ya na
gonjwa bali tukupata Uajari.

Mababilis ya Maringira, Mfano
kichumi, hasa meeme ya kifaa na hori.
Leali Seng hivyo watu bone athirile Seng
na ugonjwa hivyo wa mapenzi kuperatua
na bichumi, ambae hansi baibidi n g
imelea ya magonjwa ya cina yeyik
bali hifubakwanya Maringira

Umoi, Mfano wazee, kusata magonjwa
tafiti hivoshq kuna wazee walio heng
hivyo na hatari kubwa yekipata mago
njwa kufukoma na kawamba in reo
cijos hifubakwanya na hivyo ya kipambana
na magonjwa kwani vimezeeciea

Kwa kuhifadhiha, Magonjwa yenye
tokeeng na Maringira si hataad Seng
buliles haya yefu ya tokona na imelaa
ya magonjwa kweni hivyo ni ngeuny
kya patikilishwa na namna aya
kifayetibni huchukua muda mrefu kufa
no kenza na kifukari:

Kielelezo Na. 11.1: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 11.

Kielelezo Na. 11.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa ambaye alibainisha
kwa usahihi vyanzo vya magonjwa yasiyoambukiza. Mtahiniwa alipangilia
kazi yake katika utangulizi, mtiririko wa hoja na hitimisho; hivyo kupata
alamu za juu.

Kwa upande mwengine, asilimia 28.2 ya watahiniwa walioshindwa kujibu
swali hili kwa usahihi hawakufahamu tofauti iliyopo kati ya magonjwa ya

